# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe,
**BARAZA LA MADIWANI.**

## TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA NNE (APRILI – JUNI) MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWENYE KIKAO CHA TAREHE 11/08/2023

***Mhe. Mwenyekiti***, Kwa Mujibu wa Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa Taarifa ya Matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila robo ya mwaka. Hivyo, Taarifa hii itagusa Maeneo yafuatayo: -

1. Taarifa za Mapokezi ya Fedha za Miradi.

    1.1 Taarifa za Miradi ya Ruzuku sekondari na wadau.

    1.2 Taarifa za Miradi ya Mapato ya ndani robo ya nne.

2. Taarifa ya makusanyo kwa robo ya nne.

3. Taarifa za matukio mbalimbali katika robo ya nne.

4. Hitimisho.



CamScanner

## 1. MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI

### 1.1 MIRADI YA RUZUKU SEKONDARI NA WADAU

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Katika kipindi hiki, Halmashauri yetu ilipokea jumla ya shilingi **3,474,680,028/=** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya Miradi mbalimbali ya Maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:

- Shilingi 1,574,900,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi kupitia Program ya BOOST.
- Shilingi 1,000,000,000.00 kwa ajili ya msaada wa bajeti (Budget Support) ya Halmashauri.
- Shilingi 215,500,000.00 kwa ajili ujenzi wa miundombinu ya shule ya sekondari Bwiru Wasichana.
- Shilingi 684,280,028 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya kata ya Kiseke na ujenzi wa nyumba za waalimu shule ya sekondari Buzuruga kupitia Program ya SEQUIP

### 1.2 MIRADI YA MAPATO YA NDANI ROBO YA NNE 2022/2023

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** kwa robo ya nne, kiasi cha shilingi **934,096,178.33** ambazo ni fedha za mapato ya ndani, zilielekezwa kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo katika kata zetu kwa mchanganuo ufuatao:

i. Shilingi 148,121,000.00 kwa ajili ya kuwezesha mradi wa ufyatuaji wa tofali

ii. Shilingi 12,958,596.90 kwa ajili ya kuwezesha kufunga umeme (LT Extension Three Phase) kwenye wodi ya hospitali ya Wilaya

iii. Shilingi 2,070,000.00 kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya

iv. Shilingi 7,926,375.00 kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa ofisi za walimu na matundu ya vyoo shule mpya ya msingi Shibula

v. Shilingi 24,030,000.00 kwa ajili ya kuwezesha ukarabati wa stendi ya daladala Buzuruga

vi. Shilingi 360,000.00 kwa ajili ya kuwezesha usambazaji wa moramu kwenye eneo la Shule mpya ya Msingi Kahama

vii. Shilingi 3,820,000.00 kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa ukuta wa mawe shule ya sekondari Ibungilo

viii. Shilingi 1,812,000.00 kwa ajili ya kuwezesha ukamilishaji ujenzi wa jengo la mama na mtoto Zahanati ya Nyamwilolelwa

ix. Shilingi 69,097,034.23 kwa ajili ya kuwezesha malipo ya awamu ya pili na tatu kutokana na Halmashauri kuchelewa kulipa deni la Msingi la mkopo wa gari SM 11547 IVECO



CamScanner

x. Shilingi 20,639,000.00 kwa ajili ya kuwezesha ukamilishaji wa ujenzi katika jengo la Utawala
xi. Shilingi 27,399,600.00 kwa ajili ya kuwezesha Manunuzi ya POS machine kwa ajili ya mfumo wa TAUSI
xii. Shilingi 1,089,000.00 kwa ajili ya kuwezesha ukamilishaji ujenzi wa vyoo vipya shule ya msingi Ibungilo
xiii. Shilingi 3,929,000.00 kwa ajili ya kuwezesha Ukarabati wa vyoo shule ya msingi Ibungilo
xiv. Shilingi 3,475,000.00 kwa ajili ya kuwezesha Ununuzi wa miche ya miti na usambazaji katika vituo vya Afya
xv. Shilingi 25,976,000.00 kwa ajili ya kuwezesha uratibu wa miradi mbalimbali inayotekelezwa katika Halmashauri
xvi. Shilingi 42,987,980.00 kwa ajili ya kuwezesha uratibu wa shughuli za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2023
xvii. Shilingi 56,271,068.57 kwa ajili ya kuwezesha Malipo kwa ajili ya uzoaji taka ngumu
xviii. Shilingi 4,163,630.00 kwa ajili ya kuwezesha manunuzi ya vifaa vya umeme katika soko la Buzuruga
xix. Shilingi 4,406,000.00 kwa ajili ya kuwezesha Ukarabati wa soko la Kiloleli
xx. Shilingi 33,853,200.00 kwa ajili ya kuwezesha ukamilishaji wa jengo la Mama na Mtoto zahanati ya Chamwenda
xxi. Shilingi 1,322,600.00 kwa ajili ya kuwezesha Manunuzi ya pikipiki kwa ajili ya mfuko wa jimbo
xxii. Shilingi 2,500,000.00 kwa ajii ya kuwezesha upasuaji wa mawe barabara ya Songambele-Kigoto Kata ya Kirumba
xxiii. Shilingi 6,658,000.00 kwa ajili ya kuwezesha maandalizi ya maonyesho ya Nane Nane 2023
xxiv. Shilingi 33,273,072.63 kwa ajili ya kuchangia mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu
xxv. Shilingi 5,000,000.00 kwa ajili ya kuwezesha Ujenzi wa zahanati ya Bwiru
xxvi. Shilingi 389,598,021 kwa ajili ya malipo ya fidia katika Mradi wa Viwanja Nyafula Mtaa wa Lugeye na Sangabuye, Kangaye Sekondari
xxvii. Shilingi 1,360,000.00 kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa vifaa vya fensi kwenye Bustani ya mboga Buswelu



CamScanner

## 2.0 TAARIFA YA MAKUSANYO YA MADENI KWA ROBO YA NNE 2022/2023

***Mheshimiwa Mweyekiti,*** Katika kipindi cha Aprili – Juni 2023 Halmashauri imekusanya shilingi. 2,847,951,081 na kufanya jumla ya Mapato yote Julai 2022-Juni 2023 kuwa shilingi. 15,794,935,503 sawa na asilimia 117%.

## 3.0 TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI KATIKA ROBO YA NNE.

i. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mnamo Tarehe 18/04/2023, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Dkt. Angelina Lubala Mabula ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo ya Ilemela alikabidhi jumla ya hati 570 za umiliki wa Ardhi kwa wananchi wa Kata ya Shibula Wilaya ya Ilemela. Pamoja na mambo mengine, aliwasistiza wananchi kujenga kwa kufuata utaratibu ikiwa ni pamoja na kuwa na vibali vya ujenzi.

ii. ***Mheshimiwa Mweyekiti,*** Mnamo Tarehe 31/05/2023 Mhe. CPA. Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza alijitambulisha rasmi katika Manispaa ya Ilemela, ambapo alitaja vipaumbele vyake ambavyo ni Ulinzi na Usalama kwa wananchi na mali zao, Ushirikiano na nidhamu kazini, uimarishwaji wa ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na utatuzi wa kero za ardhi.

iii. ***Mheshimiwa Mweyekiti,*** Mnamo Tarehe 09/06/2023 aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela Mhandisi Modest J. Apolinary aliwaaga rasmi wana Ilemela na kumkaribisha Mkurugenzi mpya Wakili Kibamba Kiomoni Kiburwa, ambaye alisistiza kuwa kipaumbele chake kikubwa ni ukusanyaji wa mapato ya ndani.

iv. ***Mheshimiwa Mweyekiti,*** Mnamo Tarehe 17/06/2023 aliyekuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilemela Ndg. Said Kitinga alikabidhi rasmi ofisi kwa Bi. Mariam Msengi ambaye ni Katibu Tawala mpya wa Wilaya ya Ilemela.

v. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mnamo Tarehe 02 Mwezi Mei 2023 wanafunzi wa kidato cha sita 902 katika Halmashauri yetu walianza mitihani yao na kumaliza tarehe 22 mwezi Mei 2023, ambapo kati yao wavulana ni 255 na wasichana ni 647. Aidha, Halmashauri yetu ina jumla ya vituo 10 vya kufanyia mtihani ambapo vituo 8 ni kwa ajili ya wahiniwa wa shule na vituo 2 kwa ajili ya watahiniwa wa kujitegemea na watahiniwa wa ualimu.



CamScanner

vi. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Mnamo tarehe 15 Mwezi Mei 2023 Halmashauri yetu iliungana na wadau mbalimbali katika kuadhimisha siku ya familia duniani iliyokuwa na kauli mbiu isemayo ***"Imarisha maadili na upendo kwa familia imra".*** mdahalo uliofanyika pamoja na mambo mengine, uliwaasa na kuwakumbusha wazazi kupunguza ubize na kuboresha malezi kwa watoto.

## 5. HITIMISHO

***Mheshimiwa Mweyekiti,*** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wewe pamoja na wajumbe wote wa baraza lako kwa ushirikiano mzuri katika nyanja zote kwa kipindi chote katika robo hii.

Pia, niwashukuru wataalam wote wa Manispaa ya Ilemela kwa kusimama vyema katika nafasi zao kwa kipindi chote.

*Mheshimiwa Mweyekiti,* Naomba kuwasilisha.

Adv. Kibamba Kiomoni Kiburwa
**MKURUGENZI WA MANISPAA ILEMELA**

MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA
S.L.P. 735
MWANZA.